

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



MKUU WA TAKUKURU (M)

BARABARA YA BOMBO HOSPITALI

S.L.P. 1953,

Simu Nambari: 027-2645186,

Nukushi: 027-2647885

Barua Pepe: rbctanga@pccb.go.tz

Wavuti: www.pccb.go.tz

21105 TANZANIA

TAARIFA KWA UMMA

KOROGWE - SEPTEMBER 18, 2020

TAKUKURU MKOA WA TANGA YAOKOA SHILINGI 21,110,000.00 ZA CHAMA CHA WALIMU CHA KUWEKA NA KUKOPA WILAYA KOROGWE ZILIZOKUWA ZIMEFANYIWA UBADHIRIFU NA BAADHI YA WALIOKUWA VIONGOZI WA CHAMA HICHO

Ndugu wanahabari.

Habari za saa hizi na hongereni kwa kazi.

AWALI ya yote nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kutujaalia uhai na kutukutanisha hapa Wilayani Korogwe

TAKUKURU Mkoa wa Tanga tunapenda kuuhabarisha Umma kuhusu urejeshwaji wa fedha **Shilingi 30,580,000.00** za Chama cha Walimu cha Kuweka na Kukopa (Korogwe Teachers SACCOS) ambazo zimeokolewa na TAKUKURU Wilaya ya Korogwe na leo tarehe 18/09/2020 zitakabidhiwa kwa viongozi wa chama hicho kupitia kwa

*Barua zote zitumwe kwa Mkuu wa TAKUKURU(M), Barabara ya Bombo Hospitali, S.L.P 1953, 21105 TANGA. Unaweza pia kuwasiliana nasi kwa njia ya simu ya Bure 113, **instagram:** takukuru.tz, **Facebook:** TakukuruTz, **Twitter:** TAKUKURU.TZ, **Online TV:** TAKUKURUTV*

Mkuu wa Wilaya ya Korogwe **Mhe. Kissa Gwakisa Kasongwa**. Fedha hizo ni kati ya **Shilingi 33,647,000.00** zilizokuwa zimefanyiwa ubadhirifu na watu watatu (3) waliokuwa viongozi wa Bodi ya chama hicho. Viongozi hao ni Tugu Zakayo aliyekuwa Mwenyekiti wa Bodi, Azaria Kisse aliyekuwa Makamu Mwenyekiti na Hamisi Salum aliyekuwa mjumbe wa Bodi hiyo.

Mnamo mwezi Aprili, 2020 TAKUKURU Wilaya Korogwe ilipokea taarifa ikiwatuhumu baadhi ya viongozi wa Chama cha Walimu cha Kuweka na Kukopa kufanya ubadhirifu wa fedha za chama hicho na kwamba pamoja na juhudi zilizofanywa na bodi ya chama hicho za kuwataka watuhumiwa kurejesha fedha lakini juhudi hizo hazikuzaa matundu.

Baada ya kupokea taarifa hiyo, TAKUKURU Wilaya ya Korogwe chini ya Mkuu wa Ofisi hiyo **Bw. Raymond Katima** ilianzisha uchunguzi ili kubaini ukweli wa tuhuma hizo. Katika uchunguzi wake, TAKUKURU ilibaini watuhumiwa kufanya ubadhirifu wa kiasi cha **Shilingi 33,647,000.00** kwa kutoa mikopo hewa, kutowasilisha marejesho na michango ya wanachama, kutoa fedha benki bila kufuata utaratibu na matumizi yake kutojulikana.

Aidha, baada ya TAKUKURU kujiridhisha kuhusu ubadhirifu huo, iliwakamata watuhumiwa na kuwataka kurejesha fedha hizo. Hata hivyo, mpaka sasa watuhumiwa tayari wamerejesha fedha taslimu ofisi ya TAKUKURU Wilaya ya Korogwe kiasi cha **Shilingi 27,610,000.00** na kiasi cha **Shilingi 2,970,000.00** zimirejeshwa kwenye akaunti ya chama, hivyo kufanya fedha zote zilizorejeshwa hadi Septemba 18, 2020 kuwa **Shilingi 30,580,000.00** na kiasi kilichobakia ambacho hakijarejeshwa kuwa ni **Shilingi 3,067,000.00**.

Ndugu wanahabari.

Tunapenda kuuhakikishia umma na wakazi wa mkoa wa Tanga kwamba TAKUKURU Wilaya Korogwe itahakikisha fedha zote zilizofujwa zinarejeshwa kwenye chama husika ili ziweze kutimiza malengo yaliyokusudiwa.

Pamoja na hilo TAKUKURU inatoa rai kwa watendaji na viongozi wanaohusika na uangalizi wa uendeshaji wa Vyama vya Ushirika kuanzia Ofisi ya Mkurugenzi kupitia Idara yake ya Kilimo na Kitengo cha Ushirika chini ya Afisa Ushirika, kutekeleza wajibu wao kwa ukamilifu ili matendo kama hayo yanayorudisha nyuma juhudi za wananchi katika kujiletea maendeleo yaweze kudhibitiwa mapema.

Aidha tunaomba kuwe na ushirikiano wa karibu kati ya Ofisi hizo na TAKUKURU Mkoa wa Tanga ili iweze kusaidia kwenye utatuzi wa changamoto mbali mbali zinazozikabili vyama vya ushirika ambazo kwa uzoefu zilizo nyingi zinatokana na ubadhirifu na ufujaji wa mali unaofanywa na viongozi wa vyama hivyo - vitendo ambavyo TAKUKURU ina uwezo wa kuvishughulikia kwa mujibu wa Sheria.

Aidha, tunawaasa viongozi wa Vyama vya Ushirika, SACCOS, VICOBA na vyama vingine vya aina hiyo pamoja na wanachama wao kuzingatia maadili katika uendeshaji wa shughuli zao za kila siku na pale inapotokea baadhi yao kutokuwa waadilifu taarifa zitolewe mapema ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

Dkt. Sharifa Bungala
KAIMU MKUU WA TAKUKURU (M)
TANGA

Imetolewa TAKUKURU Wilaya ya Korogwe Septemba 18, 2020
